

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA SHINYANGA,
MHESHIMIWA ZAINAB R. TELACK KWA WANANCHI WA
MKOA WA SHINYANGA WAKATI WA MAADHIMISHO YA
SIKU YA WANAWAKE DUNIANI TAREHE 8 MACHI 2017
YALIYOFANYIKA KIMKOA KATIKA MANISPAA YA
SHINYANGA**

Kaimu Katibu Tawala Mkoa,

Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya,

Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa na Wilaya,

Waheshimiwa Wenyevititi wa Halmashauri,

Waheshimiwa Madiwani wa Mkoa wa Shinyanga,

Wakurugenzi wa Halmashauri,

Ndugu viongozi wa Dini na Mashirika yasiyo ya Kiserikali,

Watendaji wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa,

Wageni waalikwa,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana

Habari za Asubuhi!!

Ndugu Wananchi,

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia sisi sote afya na kutuwewezesha kukutana hapa kwa lengo la kuadhimisha siku hii muhimu ya wanawake Duniani.

Pia natoa pongezi zangu za dhati kwa wale wote mlioweza kuandamana na kufika hapa kwa ajili ya kuadhimisha Siku hii muhimu ya Wanawake Duniani ambayo huadhimishwa tarehe 8 Machi kila mwaka.

Ninawashukuru vikundi vyote vya sanaa waliotupatia burudani na kutoa ujumbe wenye kuelimisha jamii, kwa hakika waandaaji wa burudani hizi wamejitahidi kutoa ujumbe wa jambo lililotuleta mahali hapa. Hii inadhihirisha namna mnavyotambua umuhimu wa siku hii na shughuli ambazo zinaendana na siku hii ya leo katika suala zima la maendeleo ya Wanawake na jamii kwa ujumla.

Aidha, ninawashukuru sana wote waliochangia kwa namna moja au nyingine kufanikisha maadhimisho haya pamoja na wote tuliojumuika hapa kuadhimisha siku hii muhimu.

Ndugu wananchi,

Kupitia matukio mbalimbali waliyofanyiwa wanawake, nchi nyingi zimekuwa na maadhimisho maalumu kwa ajili ya kumkumbuka kila mwanamke duniani na kutafakari kwa kina mchango na umuhimu wake katika uwepo wa dunia na mwendelezo wa maisha.

Leo ni siku ya kutazama na kutafakari juu ya nafasi ya Mwanamke katika suala zima la maendeleo. Ni siku ya kujipima na kutathmini namna gani wanawake wamewezeshwa kujitambua na kushirikishwa katika mipango ya maendeleo ya jamii yetu kwa kushirikiana na Wanaume.

Ndugu wananchi,

Kauli mbiu ya Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Mwaka 2017 inasema **“TANZANIA YA VIWANDA: WANAWAKE NI MSINGI WA MABADILIKO YA KIUCHUMI”**. ujumbe huu unatukumbusha katika harakati za uhamasishaji na utekelezaji kwa vitendo wa Tanzania ya Viwanda, wanawake wasiachwe nyuma kwani wanamchango mkubwa kiuchumi katika kufikia lengo hili la Tanzania ya Viwanda. Wanawake wa Tanzania kupitia Serikali, Asasi, Taasisi na vikundi mbalimbali wamekuwa wakihamasishwa na

kuwezesha kufanya shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kwa mtu mmoja mmoja au katika vikundi hivyo, lengo likiwa ni kuchangia kukuza uchumi wa familia na Nchi kwa ujumla.

Aidha, Serikali kupitia wadau mbalimbali inaendelea kuwaimarisha wanawake kwenye shughuli wanazozifanya kama za ufinyanzi wa vyungu, utengenezaji wa batiki, sabuni, magodoro, ushonaji n.k. kwa kuwapa elimu na ujuzi wa namna ya kuongeza mnyororo wa thamani kwenye bidhaa mbalimbali wanazozalisha ili ziweze kupata soko kubwa hivyo kupelekea uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo ambavyo vitaongeza fursa ya ajira kwa wanawake wengi zaidi, hii itapelekea kupungua kwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI kwani muda mwingi utatumika kwenye shughuli za uzalishaji badala ya kujihusisha na masuala ya anasa.

Tanzania ni miongoni mwa Mataifa ambayo yamekuwa mstari wa mbele kutambua mchango wa mwanamke na kuthamini jitihada zake katika kuleta mafanikio na kuhamasisha mabadiliko ya jamii kwa kuzingatia masuala ya Jinsia. Serikali kwa kushirikiana na Asasi mbalimbali imekuwa mstari wa mbele katika harakati za kuimarisha, kutetea na kupigania

maslahi ya wanawake kwa kuunganisha nguvu na sera kama familia moja.

Ndugu wananchi,

Kupitia maadhimisho haya, serikali inatoa wito kwa jamii nzima kutambua kuwa ujenzi wa Taifa lolote Duniani hauwezekani isipokuwa kwa ushirikiano kati ya mwanamke na mwanamume.

Ili kuamua ni aina gani ya jamii ambayo taifa fulani limekusudia kuwa nayo, ama kiwango cha maendeleo kilichokusudiwa ni lazima kuwe na ushirikishwaji wa wanawake kwa kiwango sawa .

Ni ukweli usiopingika kuwa wanawake ni msingi wa mabadiliko ya kiuchumi maana wasiposhirikishwa na kuwezesha nchi yoyote haiwezi kuendelea. Ninawasihi kila mmoja achochee mabadiliko kwa kutoa vipaumbele katika masuala yanayowahusu wanawake katika programu na miradi mbalimbali ili kuleta usawa wa kijinsia na kuharakisha maendeleo ya watu wote kwa ujumla.

Ndugu Wananchi,

Sina budi kuwasihi wanaume kwa wanawake kushirikiana ili tuendelee kuongeza kasi ya uelewa wa masuala ya jinsia kwa lengo la kuleta mabadiliko chanya ndani ya jamii na hatimaye kuongeza kasi ya maendeleo kwa wakazi wa Mkoa wa Shinyanga.

***“TANZANIA YA VIWANDA: WANAWAKE NI MSINGI WA
MABADILIKO YA KIUCHUMI”***

Ahsanteni kwa kunisikiliza.